Jina ______________________ Nambari ya usajili ______________

Shule ______________________ Tarehe ______________

Maagizo: Maswali ya kuchagua majibu MUDA: SAA 1 DAK 40

## SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI (Alama 10)

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 1 hadi 10.**

Maisha ya jogoo huanza kama ya ndege wale wengine. Koo hutaga mayai kama ishirini hivi. Baada ya kuyaatamia kwa siku ishirini na moja, huangua vifaranga wachache kama kuna mayai viza. Yeye huangua vifaranga baada ya wiki tatu. Vifaranga hawa hukua na kuwa majogoo na makoo. Jogoo anayejifunza kuwika huitawa kipora. Huchukiwa sana na majogoo wakubwa. Kila anapojaribu kuwika hupigwa na kufukuzwa. Watu husema sauti ya "Koikoi yokoo" aitoayo jogoo anapowika lazima iwe na ujumbe ambao haufai kutolewa na vipora. Hii ndio sababu kipora hufukuzwa anapojaribu kutoa bila kibali cha majimbi wale wakubwa.

Jogoo huwika kabla ya mapambazuko. Kwanza hupigapiga mbawa zake mara mbili tatu hivi, kisha huwika. Baada ya jogoo wa kwanza kuwika, majogoo wale wengine hufuata. Sauti za "Kokoiyokoo" husikika kwa mapokezano kutoka sehemu mbalimbali. Jogoo kama baadhi ya wanyama wengine, huwa na sehemu fulani anayosimamia.Makoo wote walio katika sehemu hiyo huwa ni wake zake. Jogoo mwengine akijaribu kuingilia sehemu hiyo, vita baina yao huanza. Anayeshinda ndiye husimamia sehemu hiyo. Jogoo anapozeeka hutaga yai dogo. Hii ni ishara kuwa ameisha nguvu ya kuzalisha.

1. Maisha ya jogoo huanzia
   A. tofauti na ya ndege wengine
   B. Kama ya ndege walé wengine
   C. kama ya mnyama
   D. kama ya mtu
2. Koo hutaga mayai
   A. ishirini
   B. zaidi ya ishirini
   C. zaidi ya hamsini
   D. kama ishirini hivi
3. Vifaranga huanguliwa baada ya siku ngapi?
   A. Kumi na nne
   B. Majuma manne
   C. Majuma na matatu
   D. Siku ishirini hivi
4. Mayai viza ni mayai
   A. yale yameoza
   B. makubwa
   C. ya jogoo
   D. yale yanayofaa kuliwa
5. Kuku atagaye mayai huitwa
   A. Jogoo  B. Jimbi
   C. Koo  D. Kipora
6. Kuatamia ni kufanya nini?
   A. Kutapikia
   B. Kulalia mayai
   C. Kukalia mayai
   D. Kuzaa
7. Nani hupigwa na wengine anapojaribu kuwika?
   A. Koo  B. Jogoo
   C. Jimbi  D. Kipora
8. Jogoo huwika
   A. kabla ya mapambazuko
   B. asubuhi
   C. baada ya mapambazuko
   D. kunapopambazuka
9. Vita huzuka wakati gani?
   A. Wakati mayai yameliwa
   B. Wakati mke mmoja ametoroka
   C. Wakati jogoo mwingine amekuja eneo fulani
   D. Wakati jogoo hajawika
10. Jogoo anapozeeka
    A. huchinjwa  B. hutaga yai dogo
    C. hupigana  D. huwika

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 11-20**

Ni kweli kuwa safari ni hatua. Mambo mengi makubwa huwa na mianzo midogo midogo . Ni muhimu kwa kila kiumbe hasa binadamu kujua kuwa ni njia bora kuendeleza majukumu yao angalau madogo, kwani kidogo kidogo mwishowe kibaba hujaa. Tusitarajie kufanikiwa mara tu tuanzapo kazi au biashara za kujitafutia riziki.

Tukiangalia, kwa mfano biashara, inafaa kuanzishwa ndogo ili hasara itokeapo mtu hawezi kupata pigo kubwa. Zaidi ya hayo, atakumbwa na matatizo ya aina kadhaa ambayo atajaribu kuyahepa kwa urahisi ili mafanikio yatimie. Mambo haya yote si rahisi kuyarekebisha mtu anapoanzisha biashara au kazi kubwa.. Anaweza kula hasara ambayo yaweza kumvunja moyo na kupoteza matumaini ya kufaulu katika kazi hiyo.

Kwa wale wanaotafuta kazi ya kuajiriwa, wasitarajie kazi kubwa kubwa ambazo zitawashughulisha mno na pengine kuwa hatari. Hali kadhalika, kazi za aina hizo si rahisi kupata. Kwa hivyo, ingefaa watu kuajiriwa kazi za vyeo vya chini. Baada ya kuzipata kazi hizo, wazitekeleze vyema huku wakitia bidii. Jambo hilo litawafanya wapandishwe vyeo na kuwa watu wenye madaraka na ambao wana ujuzi wa miaka mingi. Kwani, mwenda pole hajikwai na akijikwaa haumii. Wanafunzi nao wajibidiishe masomoni tangu shule za chekechea wakipita shule za msingi na upili hadi vyuo vikuu kusomea taaluma tofauti tofauti hata ikiwa itawachukua kipindi kirefu.

**11.** Kulingana na mwandishi,
- A. mambo madogo hayawezi kuwa makubwa
- B. mambo madogo mara nyingi husababisha balaa ndogo
- C. uchache wa mali husababisha ufukara
- D. uchache wa mali hufanya watu kufanya kazi kwa bidii

**12.** Makala haya yanatueleza kuwa
- A. watu hujifunza mengi wakiwa watu wazima
- B. watu huelewa mambo vyema wakikumbana nayo
- C. watu hujifunza mengi kutokana na makosa wanayoyafanya
- D. watu hufanya kazi mbalimbali

**13.** Kwa nini wanaotafuta kazi wanashauriwa kutafuta kazi za ngazi za chini?
- A. Ili wasiwe na mishahara mikubwa itakayowaingiza katika anasa
- B. Kazi kubwa ni za watu walio na elimu za juu
- C. Ili waanze kujifunza kazi aina nyingi polepole
- D. Kazi kubwa zinahitaji ujuzi wa miaka mingi

**14.** Kwa maoni yako, ni kwa nini wanafunzi husoma hatua kwa hatua?
- A. Ili waelewe mambo mengi wanayofunzwa
- B. Ili kuwawezesha kusoma kwa miaka mingi
- C. Ni muhimu mtu kujifunza mambo taratibu
- D. Kuwawezesha kuyaelewa mambo wanayofunzwa

**15.** Maelezo ya jumla kuhusu taarifa uliyosema ni
- A. maisha ni polepole
- B. ni vigumu kupata mafanikio
- C. kuna matatizo mengi duniani
- D. mambo madogo husumbua kuliko makubwa

**16.** Ni mpango upi unaonyesha viwago vya elimu kuanzia chini hadi juu?
- A. Shule ya msingi, chekechea, shule ya upili, chuo kikuu
- B. chuo kikuu, shule ya upili, shule ya msingi, chekechea
- C. chekechea, shule ya upili, shule ya msingi, chuo kikuu
- D. Chekechea, shule ya msingi, shule ya upili, chuo kikuu



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

17. Ni methali ipi isiyofaa kulingana na habari?
A. polepole ndio mwendo
B. haraka haraka haina baraka
C. kawia ufike
D. usipoziba ufa utajenga ukuta

18. Neno **"pigo"** limetumika kwa maana ya
A. manufaa
B. aibu
C. mapato
D. balaa

19. Taaluma ni
A. ujuzi kutokana na tajiriba
B. elimu kutokana na tajiriba
C. elimu kutokana na kusoma
D. elimu kutokana na ujuzi

20. Kulingana na habari, 'kifungu 'kipindi kirefu' kinaonyesha
A. karne nyingi
B. miaka mingi
C. miezi kumi na miwili
D. siku chache

**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali kutoka 21 - 25.**

**Tobi** : Nahisi njaa jamani. Nataka kula samaki.

**Dadisi** : Umtoe wapi samaki na kiangazi hiki. Samaki ni ghali sana. Labda uende kuishi karibu na ziwa.

**Moko** : Nami ningependa kumla mamba. Nyama yake ni tamu sana

**Abiud** : Mna wazimu gani? Hamkula kishuka? Maajabu haya!

**Dadisi** : Ni ndoto kweli hizo. Baadhi ya wanyama wa majini kama vyura, kiboko na kasa hawapaswi kuliwa hata sura zao zaogofya.

**Zari** : Maisha ya siku hizi yanahitaji ujasiri. Mradi tu nyama yao isiwe sumu mwilini. Hata vyura wataliwa tu.

**Sasia** : Hapo umegonga ndipo. Chochote kisichokudhuru hakina shida

**Dadisi** : Mnyama hana hatia, auawe na nyama yake kuliwa! Hiyo sio haki. Watalii huzuru kwetu ili kuwatazama wanyama kama viboko na kasa. Mkiwala tutatoa wapi fedha za kigeni jamani!

**Buluku** : Wanyama wa majini sharti watunzwe ili binadamu wanufaike nao.

21. Mazungumzo haya yana wahusika wangapi?
A. Sita B. Saba C. Nane D. Kumi

22. Ipi maana ya **kiangazi**?
A. Msimu wa jua kali
B. Msimu wa baridi
C. Msimu wa mvua
D. Msimu wa mvua ndogo ndogo

23. Kati ya hawa wanyama ni yupi huliwa?
A. Mamba B. Simba C. Nyoka D. Samaki

24. Kisawe cha mamba ni
A. ngiri B. fuko C. ngwena D. mtambachi

25. Kulingana na mazungumzo haya kwa nini wanyama wa majini watunzwe?
A. ni kitoweo
B. ni kivutio cha watalii
C. ni hatari kwa usalama
D. wanaogofya



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**Soma kifungu kifuatacho. Kwa kila swali umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Je, umewahi kujiuliza __26__ wadudu __27__ mchwa wanavyoishi? Wadudu __28__ huishi katika makundi. Katika _29_ hiyo, utampata Malkia ambaye _30_ lake ni ___31_ tu! katika jamii hiyo _32_, utawapata walinzi _33_ kazi yao muhimu ni kuulinda _34_ wa jamii nzima. Panapotokea uvamizi, wao hujitokeza _35_ na kuuma maadui _36_ ukali kweli. Pia kuna __37___ ambao hutayarisha kichuguu. Nao hutumia __38___ mkubwa sana. Kichuguu hujengwa __39___ na vyumba mbalimbali ___40___ wakitumia udongo na mate pekee.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **26.** A. vilevile | B. aina | C. walivyo | D. jinsi |
| **27.** A. akina | B. waitwao | C. hao | D. kama |
| **28.** A. huyo | B. wale | C. hawa | D. wengi |
| **29.** A. vikundi | B. hundi | C. mikusanyiko | D. makundi |
| **30.** A. jukumu | B. kazi | C. nia | D. haja |
| **31.** A. uzao | B. kuzaa | C. uzalishaji | D. huzaa |
| **32.** A. hiyo | B. hii | C. iyo | D. ile |
| **33.** A. ambazo | B. ambamo | C. ambaye | D. ambao |
| **34.** A. salama | B. amani | C. usalama | D. umoja |
| **35.** A. tayari | B. kivita | C. wajenzi | D. hiari |
| **36.** A. kwa | B. wa | C. kuwa | D. na |
| **37.** A. wajuzi | B. ujenzi | C. wajenzi | D. watengenezaji |
| **38.** A. mjusi | B. ujuzi | C. ujusi | D. mjuzi |
| **39.** A. ukiwa | B. vikiwa | C. kikiwa | D. wakiwa |
| **40.** A. wakiwa | B. humo | C. na | D. huko |

**Jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.**

**41.** Nauli ni malipo ya
A. kusafiria B. shule
C. mganga D. kuoa

**42.** Katika maandishi, aya ni
A. fungo la maneno mengi
B. fungu la silabi
C. fungu la sentensi
D. fungu la maneno yenye maana

**43.** **Kamilisha methali hii**
Kukopa kunazaa ___________
A. utajiri B. umaskini
C. umaarufu D. uharibifu

**44.** **Tegua kitendawili hiki**
Nyama nje ngozi ndani
A. embe B. firigisi
C. papa D. mahindi

**45.** Tazama mchoro ufuatao. Jina la mchoro huu Unapatikana katika ngeli gani?



A. A-WA
B. I-ZI
C. KI-VI
D. U-I

**46.** Tambua nomino katika sentensi hii.
Shangazi yangu anafua nguo zetu
A. Shangazi
B. Yangu
C. Zetu
D. Anafua

**47.** Chagua sentensi iliyo katika hali timilifu.
A. Mwembe ulikatwa
B. Mwalimu atawasili baadaye
C. Kaka ameenda shambani
D. Dada anafanya kazi ya ziada

**48.** Onyesha kitenzi katika sentensi hii
**Kitabu changu kilipotea jana**
A. jana B. kilipotea
C. changu D. kitabu

**49.** **Ni nini maana ya methali**
"Mpanda ngazi hushuka"?
A. Ngazi ni chombo cha kushuka
B. Mwenye ngazi anashuka
C. Mtu anatumia ngazi kushuka
D. Mtu mwenye cheo anaweza shuka

**50.** Neno **makiwa** huambiwa mtu
A. aliyefiwa
B. mtu aliyefariki
C. anayeenda kulala
D. aliyefaulu



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com